# Kristo 5



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


BAADA YA KUTEUWA WAFUASI WAKE, YESU ALIENDELEA KUSAFIRI, KUPONYA NA KUFUNZA.
HERI WALIO MASKINI WA ROHO; MAANA UFALME WA MBINGUNI NI WAO!
HERI WENYE HUZUNI; MAANA HAO WATAFARIJIWA!
HERI WENYE UPOLE; MAANA WATAIRITHI NCHI!
HERI WENYE NJAA NA KIU YA HAKI!
MAANA HAO WATASHIBISHWA!
HERI WENYE REHEMA; MAANA HAO WATAPATA REHEMA!
HERI WENYE MOYO SAFI; MAANA HAO WATAMWONA MUNGU!
HERI WAPATANISHI; MAAN WAO WATAITWA WANA WA MUNGU!
HERI WENYE KUUDHIWA KWA AJILI YA HAKI; MAANA UFALME WA MBINHUNI NI WAO!
HERI NYINYI WATAPOWASHUTUMU NA KUWAUDHI NA KUWANENEA KILA NENO BAYA KWA UONGO KWA AJILI YANGU!
FURAHINI! KWA MAANA NDIVYO WALIVYOWAUDHI MANABII!
THAWABU YENU NI KUBWA MBINGUNI!
MATHAYO 5:1-12; LUKA 6:17-23


NYINYI NI CHUMVI YA DUNIA!
LAKINI CHUMVI IKIWA IMEHARIBIKA, ITIWE NINI NDIO IKOLEE?
HAIFAI TENA! ITATUPWA NJE NA KUKANYAGWA NA WATU!
NYINYI NI NURU YA ULIMWENGU!
NA UNAFANYA NINI NA MWANGAZA? WAUWEKA UNAPOWEZA KUNGAA NA KUANGAA KUWAPA WATU MWANGAZA!
KWA HIYO, ACHA MWANGA WENU UNGAE KWA WATU, NDIPO WATU WAMSIFU BABA YENU ALIYE MBINGUNI
MSIDHANI NIMEKUJA KUITANGUA TORATI NA MANABII!
LA . . .
ILA KUZITIMIZA!



MATHAYO 7:24-29, 8:5-7; LUKA 6:47- 49, 7:1-6






MATHAYO 8:8-13; LUKE 7:6-10


NJE YA JIJI LA NAIN.
TAFADHALI! TUNA MWANDAMANO WA MAISHI WAJA!
TAFADHALI MSITUZUIE!
SUBIRI! TAFADHALI, WACHA!
MAMA MPENDWA, USILIE.
LAKINI MWANANGU... MWANZO MUME WANGU, SASA PIA MWANANGU!
INUKA!
ONDOKA HAPO!
AFANYA NINI?
ANA KICHAA!!
NI . . . NI . . . KIVIPI?
HAIWEZEKANI!
NI MUNGU TU AWEZAYE KUYAFANYA HAYA!
NABII YU KATI YETU!
MSIFU MUNGU!
MSIFU!
"KWA HIYO WATU WALIVOANZA KUMSIFU MUNGU NA SASA KILA MTU ANAYAZUNGUMZIA MAMBO HAYA, YOHANA! NATAMANI --"

LUKA 7:11-18






MATHAYO 11:2-6; LUKA 7:18-23




MATHAYO 11:7-15; LUKA 7:24-30






MATHAYO 11:16-19; LUKA 7:29-37


SAMAHANI.
MANUKATO, BWANA.
NIRUHUSU NIIOSHE MIGUU YAKO.
NA KAMA ANGEKUA NABII KAMA ASEMAVYO, ANGEJUA VILE MWANAMKE HUYU ALIVYO MZINIFU!
ACHA NIKUAMBIE KITU.
JAMAA MMOJA ALIDAI DENARII MIA TANO NAYE ALIDAIWA NA MWENGINE HAMSINI.
HAKUNA ALIYEKUWA NA PESA ZA KUMLIPA KWA HIYO AKAYAFUTA MADENI.
NI NANI ATAKAYEMPENDA MKOPESHAJI ZAIDI?
ALIYEDAIWA ZAIDI.
ANAIOSHA MIGUU YANGU KWA MAPENZI; YUAJA KWANGU NA IMANI.
DHAMBI ZAKO ZIMESAMEHEWA.
ENDA. IMANI YAKO IMEKUOKOA. ENDA KWA AMANI.
MPAKA WASEMEHEA DHAMBI?
KILA KITU NIMEPEWA NA BABANGU.


YESU NA WAFUASI WAKE KUMI NA WAWILI WALIENDELEA KUSAFIRI KIJIJI HADI KIJIJI.
MAGDALA KWENYE UFUO WA MAGHARIBI WA BAHARI LA GALILAYA.
ULIZA NA UTAPEWA!
ANAYETAFUTA ATAPATA!
NILIMSKIA AKIYAFUNZA HAYA MILIMANI NJE YA GALILAYA!
WE NAWE! HAUBADILI NIA HIVI SASA!
LA!!!
SITABADILI!!!
MWEKE KANDO!!!
NJOO!
TAHADHARI, BWANA!
KAA KANDO!!! ONDOKA!!
MWANAMKE HUYU...
AMEPAGAWA! ALISKIA KUKUHUSU!
ALIKUA DHAHIRI, ALISEMA TUMLETE KWAKO. ILA TULIPOMLETA...


LA.
SIENDI KOKOTE.
LAKINI WEWE UTAONDOKA.
NI WETU!
ALITUALIKA!
HAUKARIBISHWI TENA.
ALIKUJA KWANGU.
UTAMUACHA.
*SASA!!!*
LUKA 8:2


YESU.
NILIJUA. NILISIKIA ALICHOFANYIA WENGINE NIKAJUA.
ASANTE.
ASANTE SANA.
NI WAKATI WETU KUSONGA MBELE.
BWANA? JINA LANGU NI MARIA.
NATAKA KUJA NAWE!
WAKARIBISHWA SANA MARIA WA MAGDALA.



LUKA 8:2


NA WAFUASI WAKIMFUATA PAMOJA NA WANAWAKE KADHAA WALIOKUWA WAMEPONYWA NA KUTOLEWA MAPEPO --
-- YESU ALIENDELEA NA HUDUMA YAKE.
WAFUASI WA YESU, WAKIWAMO WANAWAKE, WALISAIDIA HUDUMA YAKE KUTOKA KWA MALI YAO WENYEWE.
YESU ALIPOSAFIRI MANENO KUHUSU MATENDO YAKE PIA YALIENEA.


MAMA! MAMA!
YWAJA HAPA!
NANI?
KAKA YETU!


YESU.
MAMA, UMATI UNAMFUATA TOKA KIJIJI KIMOJA HADI CHENGINE!
WANASEMA ANATOA MAPEPO!
MAMA, AMESHIKWA NA KICHAA KABISA!
ITABIDI TUMKATAZE!






MATHAYO 12:22-23; MARKO 3:20


MAMA... BABA... NAWAONA!
LA! MUONDOKEE MZUSHI HUYU!
KAMA YUATOA MAPEPO NI KUPITIA BWANA WAKE!
KUPITIA BEELZEBUB, MKUU WA MAPEPO, NDIO ANA MAMLAKA YA KUFANYA HIVI!
BILA SHAKA AMEPAGAWA NA BEELZEBUB MWENYEWE!
UNA UHAKIKA WASEMA NINI?
SHETANI ATAMTOAJE SHETANI?
JE, NYUMBA ILIYOTENGANA YAWEZA KUSIMAMA?
JIJI? UFALME?
LA! NA SHETANI PIA AKIJIPINGA MWENYEWE PIA HAWEZI KUSIMAMA!
KAMA NATOA MAPEPO KWA NGUVU ZA BEELZEBUB MWAFANYAJE?
KAMA NAYATOA MAPEPO KWA ROHO WA MUNGU BASI UFALME WA MUNGU UMEWADIA!
ANAYENIPINGA HAYUKO NAMI!
ASIYE KUSANYA NAMI ANATAWANYA!
MTI WAJULIKANA KWA MATUNDA YAKE!
MTU MZURI HULETA MAZURI KUTOKANA NA UZURI ULIO NDANI YAKE; MTU MUOVU, VITU VIOVU!
NA SIKU ITAFIKA WAKATI WATU WOTE WATAHUKUMIWA!


TUPE ISHARA!
HAPA! ISHARA YA YONA SIKU TATU KWENYE TUMBO LA SAMAKI!
PIA MWANA WA ADAMU ATAKUA KWENYE ARDHI SIKU TATU!
WATU WA NINEVA WANGEKUHUKUMU KWA KUWA WALITUBU JUU YA FUNZO LA YONA!
LAKINI MNA MMOJA KATI YENU ALIYE MKUU ZAIDI!
MALKIA WA SHEBA ANGEWAHUKUMU MAANAKE ALISIKIZA HEKIMA YA SULEIMAN!
NA SASA MMOJA MKUU KULIKO SULEIMAN YU NANYI!
"MKUU KUMSHINDA SULEIMAN"?
ANA KICHAA!
SAMAHANI KIJANA.
WAEZA KUPENYA KATI YA UMATI UMPE MWALIMU UJUMBE TOKA KWA MAMAKE NA NDUGUZE?
BILA SHAKA!
MWALIMU! MAMAKO NA NDUGUZE WAKO NJE!
WATAKA KUKUONA!
MAMANGU NI NANI? KAKA ZANGU NI AKINA NANI?
KAKA ZANGU HAWA!
YEYOTE ATIMIZAYE NIA YA MUNGU NI MAMANGU NA KAKANGU NA DADANGU!
YEYOTE ASKIZAYE NENO LA MUNGU NA KULITENDA NI MAMANGU NA KAKANGU NA DADANGU!
AMECHAN-GANYIKIWA!
ANAAMINI ANACHOROPOKWA!
NJOO MAMA TURUDI NYUMBANI!




MATHAYO 13:1-23; MARKO 4:1-20; LUKA 8:4-15


YESU ALISEMA MAFUMBO MENGI.
UFALME WA MBINGUNI NI KAMA MPANZI ALIYEPANDA MBEGU NZURI KWA KIWANJA CHAKE LAKINI ADUI YAKE AKAJA KUWEKA MIIBA KATI YA MBEGU!
WAFANYA KAZI WALIULIZA WAVUTE MIBA LAKINI MPANZI ALIKATAA.
ACHA IWE MPAKA MAVUNO KISHA TUCHAGUE VIZURI.
HAKUNA AWASHAYE TAA NA KUIWEKA CHINI YA KITANDA!
LA, UNAIWEKELEA WATU WATAKAPOONA MWANGA!
FAHAMU HIVI! HAKUNA KILICHOFICHIKA KISICHOTOKEA KWENYE MWANGA!
UFALME WA MBINGUNI NI KAMA MBEGU YA HARADALI ILIYOPANDWA KWENYE KIWANJA.
NDIO MBEGU NDOGO ZAIDI, LAKINI YAMEA KUWA MMEA MKUBWA ZAIDI SHAMBANI!
UFALME WA MBINGUNI NI KAMA HAZINA ILIYOFICHWA KWA KIWANJA.
MTU ANGALIKIONA ANGEFANYA NINI?
ANGENUNUA KIWANJA!
NDIO! ANGEUZA KILA KITU ILI ANUNUE KIWANJA HICHO!
MWAELEWA MAFUMBO YANGU?
BILA SHAKA!
VYEMA! KWA KILA MWALIMU ALIYEFUNZWA JUU YA UFALME WA MBINGUNI--
--NI KAMA MWENYE NYUMBA ATOAE HAZINA MPYA NA NZE KUTOKA KWENYE HAZINA!
ALIPOMALIZA KUFUNZA MAFUMBO PALE, ALIENDA MBELE.
MATHAYO 13:24-53; MARKO 4:21-34




MATHAYO 8:23-26; MARKO 4:35-38; LUKA 8:22-24


KIMYA, UPEPO!
AMANI, MAWIMBI!
TULIA!!!
NI MTU WA AINA GANI?
PIA UPEPO NA MVUA NA MAZIMBI VYAMTII!
UPANDE MWENGINE, ENEO LA WAGERASI.




MATHAYO 8:28-29; MARKO 5:2-8; LUKA 8:27-29


UTAONDOKA NDANI YA MTU HUYU.
TAFADHALI! APA KWA MUNGU HAUTATUTESA!
WAITWA NANI?
JESHI.
MAANA TU WENGI.
TAFADHALI, TUAMURU TUWAINGIE NGURUWE WALE!
KAMA NI LAZIMA UTONDOE FANYA HIVYO!
ENDENI BASI!
AAAAHHHHH




MATHAYO 8:32-34; MARKO 5:13-17; LUKA 8:33-37






MATHAYO 8:34; MARKO 5:17-20; LUKA 8:37-39



# HADITHI YA MTAWALA

## "ZAWADI"




ALINIWEKA MFALME KWENYE WOSIA WAKE WA TANO.
LAKINI SIKU TANO KABLA HAJAFA ALIBADILISHA WOSIA WAKE TENA!
KAMA MWILI WAKE MZEE MCHOVU UNGEKUFA WIKI MOJA MAPEMA NINGEKUWA MAFALME!
LAKINI LA!
BADALA YAKE ALIMTAJA KAKANGU ARCHELAUS AWE MFALME!
KAKANGU FILIPO NA MIMI TUKAWA WATAWALA!
MTAWALA ANAYETAWALA ROBO YA UFALME!
NILIPASWA KUWA MFALME!
WAHITAJI CHOCHOTE MPENZI?
NASHKURU MALIKI AGUSTUS ALITOA UFALME AKAMFANYA KAKANGU MTAWALA BADALA YAKE.
MTAWALA WA NCHI. KWA HIYO HAKUWA MFALME LAKINI ALIKUWA NA MAMLAKA ZAIDI YANGU!
GALILAYA NA PEREA.
NINI MPENZI?
NAFAA NIITAWALE YOTE SIO HILI ENEO DOGO TU!
NAHITAJI KITU CHA KUNITOA MAWAZO.
PENGINE MBATIZAJI!
HAPANA!
KWA NINI WAPENDELEA KUUSIKIZA UPUZI HUU?
ANIFURAHISHA!
HANIFURAHISHI!
BILA SHAKA NILIJUA ALICHOKIMAANISHA. HERODIAS AIKUWA MKEWE KAKANGU.
ALIMTALIKI FILIPO AKANIOA MIMI. MPATIZAJI YOHANA HAKUPENDEZWA.
UMEWAFANYIA MENGI WATU HAWA. KUJENGA MIJENGO NA MIJI...
ULIMSHAWISHI PILATO ABOMOE SANAMU WAYAHUDI WALE WALIZIDHANIA MIUNGU!
HAUITAJI KUSKIZA YOHANA AKIROPOKWA JUU YA NDOA YETU ZINIFU!
WAHITAJI KITU CHA KUFURAHISHA ZAIDI!



ALIKUWA MWEREVU, MKE WANGU.
MWEREVU SANA NADHANI.
WAONA NINAYOSE-MA?
KILE WAHITAJI!
MPAKA WATU WAGUNDUE USHURU WAO UMETUMIKA KUFANYA SHEREHE AMBAYO HAWANGEPENDELEA!
SAHAU JUU YA WATU KWA MDA EH?
WATU WANICHUKIA!
WANANICHUKIA SABABU YA BABANGU.
KWA SABABU NIKO CHINI YA ROMA!
KWA SABABU SIFATIZII DINI YAO KWA USAWA!
WANICHUKIA MAANAKE HAWAWEZI KUWA NA MFALME KAMILI!
MIMI, MUME MPENDWA SIKUCHUKII.
WAWEZA KUKAA HAPA UKAHUZUNIKA, UKIPENDELEA.
NITAFURAHIA SHEREHE HII.
KUNA SABABU MOJA TU NILIJALI WATU WANAVYOFIKIRIA.
WATU WAKIWA NA RAHA KAZI YANGU NI RAHISI.
WATU WASIPOKUWA NA RAHA KAZI YANGU SIO RAHISI.
NA WATU WASIO NA RAHA LABDA YAMAANISHA MWISHO WA MAMLAKA YANGU.
NAPENDA KILE MAISHA HAYA YAMENIPA.
NA ITACHUKUA JAMBO MOJA KUMALIZA MAISHA YANGU HAYA...
DENSI!
NAAM, TUCHEZEE!


CHEZA SALOME!
MWANGALIE!
SALOME.
BINTIYE MKE WANGU.
JE HERODIAS ALIKUWA MREMBO HIVI UJANANI?
NDIO! CHEZA SALOME!


MREMBO, SIO?
ACHEZA... VIZURI.


MARIDADI KABISA!
AJABU!
HUKO KUCHEZA!
NI MREMBO, MSICHANA HUYU SALOME.
NIMEFURAHIA.
HUKO KUCHEZA, HIYO TAMASHA, HUO UREMBO, WASTAHILI ZAWADI.
TAJA TU.
CHOCHOTE UTAKACHO TOKA KWANGU NI CHAKO!
CHOCHOTE!
NIPE MDA NIWAZE MFALME HERODE.
"MFALME." NDIO, SAA ZENGINE WATU HUNIITA "MFALME," LAKINI MIMI SIO MFALME.
ANA UZOEFU WA KUCHEZA?
NI WA AJABU, SIO?
WAFAA KUWA NA SHEREHE HIZI MARA KWA MARA!
NIMEJUA, HERODE MKUU!


NI NINI?
KITU KIMOJA TU.
YOHANA MBATIZAJI.
NILETEE KICHWA CHAKE.
KWENYE SINIA.
HAPANA.
ALIULIZIA KITU KIMOJA KILICHO CHANGU...
...AMBACHO SINGEPEANA.
LAKINI HAIKUWA HAMU YA SALOME.
KUMUUA MTU KAMA YEYE INGESABABISHA SHIDA ZAIDI NA WAHIBRANIA.
LAKINI NILIAHIDI... MBELE YA WATU WOTE...


SAWA, NITAFANYA!
MUITE KAPTENI WA WALINZI!
MWAMBIE AMLETE MFUNGWA! AKATE KICHWA CHAKE! AKILETE HAPA!
KWENYE SINIA.
KAMA MFALME - AU MTAWALA - WAWEZA KUTUMIA WAKATI NA PESA NYINGI KUWAFANYIA WATU MAMBO MAKUBWA--
--LAKINI YACHUKUA KITU KIMOJA KIDOGO KUHARIBU HAYO.
KICHWA CHA NABII.
KWENYE SINIA.
ALIELEWA MATOKEO ALIVODHIBITI HILI?
SIKU ZILIPITA NA HABARI YA KITENDO CHANGU KUENEA.
WENGINE WALIJALI, WENGINE HAWAKUJALI.
KWA WALE WALIONICHUKIA TAYARI ILIWAPA SABABU TOSHA ZAIDI.
MIMI SIO MFALME WAO.
ILA NAPENDA VITU NINAVYOPATA KWA MAISHA HAYA, NA KAMA NITAVISHIKILIA--
--BASI ITABIDI NIPATE KITU CHENGINE NTAKACHOFANYA KUWAFURAHISHA.
KITU KITATOKEA, NINA UHAKIKA.

"THE BIBLE EXPLAINED IN EVERY LANGUAGE."





SUPERBIBLE.TV